

جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية المجالس بالزلفي

مشروع تعلم الإسلام - أحكام الصلاة - سواحيلي

Samo la 3

الدرس الثالث

NYAKATI ZA SWALA.

- Wakati wa swala ya adhuhuri ni kuanzia kumili jua kuelekea upande wa magharibi mpaka kuvuli kulingana sawa mfano wake kwa urefu.
- Wakati wa swala ya alasiri ni kuanzia kulinga kivuli mfano wake mpaka kuzama kwa jua.
- Wakati wa swala ya magharibi ni kuanzia kuzama kwa jua mpaka kupotea kwa mawingu mekundu, nao ni wekundu unaojitokeza wakati wa kuzama kwa jua.
- Wakati wa swala ya Ishai ni kuanzia yanapopotea mawingu mekundu mpaka nusu ya usiku.
- Wakati wa swala ya alfajir ni kuanzia kuchomoza kwa alfajiri mpaka kuchomoza kwa jua.

NYAKATI ZILIZO KATAZWA KUSWALI.

Kuna nyakati ambazo zimekatazwa kuswali ndani ya nyakati hizo;

- Baada ya swala ya alfajir mpaka kuchomoza kwa jua mpaka lifike kiasi cha mkuki.
- Wakati jua likiwa katikati wakati wa mchana mpaka limili upande wa magharibi.
- Baada ya swala ya alasir mpaka kuzama kwa jua.

Lakini inafaa kutekeleza baadhi ya swala katika nyakati hizi zilizokatazwa mfano swala zenye sababu maalumu kama vile Tahiyatul masjid (sunnah ya kuingia msikitini), swala ya jeneza, swala ya kupatwa kwa jua, rakaa mbili za twawifu, rakaa mbili za udhu na mfano wake.

Vile vile inafaa kukidhi swala za faradhi zilimpita mtu kwenye nyakati hizi, Mtume (saw) anasema:

لقوله ﷺ : ((من نسي صلاةً أو نام عنها ، فكفارتها أن يُصلِّيهَا إِذَا ذُكِرَهَا)) [منظر عليه: 597، 684]

(Mtume (saw) anasema: Mwenye kuisahau swala au akalala, basi kafara lake ni kuiswali hiyo swala pindi atakapo ikumbuka) (Ameipokea Imamu Bukhar na Muslim :597, 684).

Kadhalika anaweza kuikidhi sunnah ya alfajir zile rakaa mbili kabla ya alfajir zikiwa zimempita katika kuzitekeleza kwa wakati wake.

SEHEMU AMBAZO HAZIFAI KUSWALI NDANI YAKE.

Sehemu ambazo hazifai kuswali ndani yake ni;

- Makaburini kwa kauli yake mtume (saw) aliposema:

((الأرض كلها مسجدٌ ، إِلَّا الْحَمَامُ وَالْمَقْبَرَةُ)) [رواه الحمسة ، وهو حديث صحيح]

(Ardhi yote ni msikiti, isipokuwa chooni na makaburini) (Imepokelewa na wapokezi watano nayo ni hadithi sahihi).

Ama swala ya jenenza inafaa kuswaliwa makaburini bila ya tatizo lolote kwani haina rukuu wala kusujudu, lakini swala za kawaida haifai kuswali makaburini.

- Kuswali kuelekea makaburini, kutokana na hadithi Abu Marthad Alghanawiy (R.A) anasema, alimsikia mtume (saw) akisema:

فَعَنْ أَبِي مَرْثَدِ الْغَنَوِيِّ - رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ - قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ - رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ - يَقُولُ: ((لَا تَصْلُوَا إِلَى الْقَبْوَرَ، وَلَا تَجْلِسُوا عَلَيْهَا)) . [رواه مسلم: 973]

(Msiswali kuelekea makaburini, wala msikae juu ya makaburi) (Ameipokea Imamu Muslim : 973).

- Kuswali kwenye zizi la ngamia, kama vle haifai kuswali sehemu ambazo kuna najisi.